

Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini

Mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ya mwaka 2007 (NAPA) inayolenga kuchukua hatua za haraka kuhimili mabadiliko ya tabianchi nchini.

Lengo kuu la mradi ni kuongeza uvumilivu wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini kwa kuimarisha mifumo ikolojia na kuwezesha jamii kuwa na njia tofauti za kujipatia mahitaji.

Mradi unatekelezwa katika Mikoa minne ya Tanzania Bara na Mkoa mmoja Zanzibar. Mikoa hiyo ni Manyara (Wilaya ya Simanjiro - Tanzania Bara), Mkoa wa Dodoma (Wilaya ya Mpwapwa - Tanzania Bara), Mkoa wa Morogoro (Wilaya ya Mvomero - Tanzania Bara), Mkoa wa Shinyanga (Wilaya ya Kishapu - Tanzania) na Kaskazini-A, (Kaskazini -Unguja).